

# TUME YA HUDUMA KWA WALIMU



## MKATABA WA UTOAJI HUDUMA

(ULIOREKEBISHWA 2017)

**Mkataba huu ni thibitisho la kujitolea kwetu, kuwahudumia wateja wetu kwa muda maalum. Kulingana na Katiba ya Kenya 2010, Sheria ya Tume ya Huduma kwa Walimu 2012, Kanuni na Taratibu za Kufuatwa na Walimu (2015), Kanuni za Mwongozo wa Maadili Mema ya Walimu (2015) na sheria nyinginezo husika.**

**Anwani:**

*TSC House,*

*Barabara ya Kilimanjaro, Upper Hill*

*Private Bag, 00100*

*Simu 020 2892000*

*Nairobi, Kenya*

*Barua Pepe : info@tsc.go.ke*

*Tovuti : www.tsc.go.ke*

**Ruwaza**

Kutoa huduma ya kufundisha yenye mabadiliko ya kuboresha elimu.

**Lengo**

Kuitaalamikisha huduma ya ufundishaji iwe bora na yenye maendeleo.

**Maadili ya Msingi**

Tume itasisitiza maadili yafuatayo;

- a) **Utaalamu**
- b) **Kuwashughulikia wateja wake**
- c) **Uadilifu**
- d) **Ubunifu**
- e) **Ushirikiano**

**TUME YA HUDUMA KWA WALIMU  
MKATABA WA UTOAJI HUDUMA**

<b>NAMBAJI</b>	<b>HUDUMA TUNAZOTOA</b>	<b>MAJUKUMU/MAHITAJI</b>	<b>MALIPO</b>	<b>MUDA</b>
1.	Huduma utembeleapo afisi za TSC	Kutaka huduma	Hakuna malipo	Utahudumiwa katika muda wa dakika 10
2.	Majibu ya barua kutoka kwa Tume	Wasilisha ombi kwa njia ya maandishi	Hakuna malipo	Muda usiozidi siku 14
3.	Usajili wa walimu	Jaza fomu ya usajili kwa ukamilifu katika mtandao kisha uiwasilishe	Kshs. 1000	Muda isiozidi siku 30
4.	Uajiri wa walimu	Wasilisha ombi kulingana na tangazo lililochapishwa	Hakuna malipo	Kuthibitisha kupokea ombi lako, kwa muda usiozidi siku 14. Matokeo ya mahojiano yatawasilishwa kwa muda usiozidi siku 15
5.	Uhamisho wa walimu	Wasilisha fomu ya maombi iliyojazwa kikamilifu	Hakuna malipo	Kuthibitisha kupokea ombi lako, kwa muda usiozidi siku 14 na kuwasilisha uamuzi wa Tume kwa siku 90
6.	<b>Ugawaji wa kazi kwa walimu</b>			
	i. Baada ya kuajiriwa	Jaza fomu ya ajira	Hakuna malipo	Barua ya ajira kutumwa kwa muda usiozidi siku 30

	ii. Baada ya likizo	Wasilisha ombi, siku 30 kabla ya likizo kumalizika	Hakuna malipo	Kwa muda wa siku 7
	iii. Uteuzi kwa nyadhifa za uongozi	Wasilisha ombi kulingana na tangazo lililochapishwa	Hakuna malipo	Kuthibitisha kupokea kwa ombi kwa muda usiozidi siku 14 na kumteua aliyefuzu kwa muda usiozidi siku 30
7.	<b>Kupandishwa mamlaka</b>			
	i. Kupitia mahojiano	Wasilisha ombi kulingana na tangazo lililochapishwa	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi miezi 3
	ii. Ukitimiza miaka 3 baada ya kuajiriwa	Wasilisha ombi siku 30 kabla ya muda wa makataa	Hakuna malipo	Siku 30
8.	<b>Kesi za kinidhamu</b>			
	i. Uamuzi wa kesi	Wasilisha taarifa ya utetezi wako kwa muda usiozidi siku 21 baada ya kusimamishwa kazi	Hakuna malipo	Uamuzi wa kesi kutolewa kwa muda usiozidi miezi 3 baada ya usajili wa kesi
	ii. Kutathmini kesi	Wasilisha ombi kwa muda usiozidi siku 90 kutoka kwa tarehe ya kuandikwa kwa barua ya uamuzi wa kesi yako	Ksh.2000	Kwa muda usiozidi miezi 3
9.	Malipo ya mishahara na kutoa hati za mishahara kwenye	Kufanya kazi uliyotengewa	Hakuna malipo	Kufikia siku ya mwisho wa mwezi

	mtandao			
10.	<p>Kutayarisha marupurupu wakati wa kuondoka kutoka kwa huduma ya Tume</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>i. Kustaafu kwa Lazima</li> <li>ii. Kustaafu Mapema kwa Hiari</li> <li>ii. Kujiuzulu kwa sababu za Kindoa</li> <li>iv. Kustaafu kwa sababu za Kiafya</li> <li>v. Malipo baada ya Kifo</li> </ul>	Wasilisha ombi kwa fomu zilizoidhinishwa na uambatanishe na stakabadhi maalum zinazopatikana katika afisi zetu za Kaunti/Kaunti Ndogo	Hakuna malipo	Kwa muda usiozidi miezi 3
11.	Kushughulikia Malalamishi na Maafikiano	Malalamishi yaliyoandikwa	Hakuna malipo	Anzisha utaratibu wa maafikiano kwa muda usiozidi siku 7